**HOTUBA YA NAIBU WAZIRI WA MAJI**
**MHE. JUMAA HAMIDU AWESO (MB)**

**WAKATI AKIFUNGUA MKUTANO MKUU WA WATENDAJI WAKUU WA SEKTA YA MAJI TANZANIA BARA KWA NIABA YA WAZIRI WA MAJI.**
**19 Desemba, 2019**

---

**Prof. Kitila Mkumbo**, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji,

**Eng. Anthony Sanga**, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji,

**Wakurugenzi wa Idara** na **Wakuu** wa **Vitengo**, Wizara ya Maji,

**Bw. Mchany Nsanjigwa**, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA)

**Eng. Clement Kivegalo**, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)

**Dkt. Omari Karia**, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Maji

**Wenyeviti wa Bodi** wa Mamlaka za Maji safi na Usafi wa Mazingira

**Maafisa wa Maji** wa Bodi za Mabonde ya Maji Nchini

**Wakurugenzi Watendaji** wa Mamlaka za Maji,

Wadau wa Maendeleo

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

**Habarini za asubuhi!**

Awali ya yote niombe nianze kwanza kwa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwepo mahali hapa siku ya leo. Ninawashukuru pia ninyi viongozi wa sekta ya maji kutoka nchi nzima kuhudhuria mkutano huu muhimu kwa wingi namna hii.

Kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa na wananchi wa Dodoma, ninawakaribisha Dodoma, ambayo ndipo yalipo makao makuu ya nchi na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwakikishie kuwa Dodoma ni shwari na tulivu na kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa.

**Ndugu Washiriki,**

Ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli** kwa kuendelea kuniamini mimi na viongozi wenzangu katika kuingoza Wizara hii yenye umuhimu mkubwa kwa jamii nan chi kwa ujumla. Ninamshukuru sana Waziri wetu wa Maji, **Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa** ambaye anaendelea kutupa uongozi mzuri katika wizara yetu, na hasa katika eneo la usimamizi wa miradi ya maji.

Ninawashukuru Katibu Mkuu **Prof. Kitila Mkumbo**, Naibu Katibu Mkuu **Eng. Anthony Sanga** na watengaji wote wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri ya kusimamia shughuli za wizara na msaada mkubwa wanaotupa mimi na Naibu Waziri katika kuiongoza sekta hii muhimu kwa maisha na maendeleo ya watanzania.

Kwa njia ya pekee kabisa ninachukua nafasi hii kumpongeza sana **Eng.Antony Sanga** kwa kuonwa, kuaminiwa na kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu. Uteuzi wa Eng. Sanga umethbitisha usemi wa Kiingereza usemao: ***Hard work pays!*** Hakuna shaka kwamba kazi nzuri aliyoifanya kanda ya ziwa katika kusimamia miradi ya maji ndiyo iliyomfikisha hapa.

Ninaomba mniruhusuni pia nitumie fursa hii adimu na adhimu kuwashukuru ninyi nyote kwa kazi kubwa mnayoifanya katika kuisimamia na kuiendesha sekta ya maji katika nafasi zenu mbalimbali. Nyie ndiyo mnaoibeba wizara na serikali kwa ujumla katika sekta ya maji. Tunawapongezeni na kuwshukuruni sana kwa kazi zenu kubwa na nzuri.

Na kwa njia ya kipekee kabisa niwashukuru ndugu zetu wa RUWASA, chini ya uongozi mahiri wa Mkurugenzi Mkuu, **Eng. Clement Kivegalo**. Pamoja na uchanga na upya wao, RUWASA wameanza vizuri na kwa sasa ndio tegemeo letu la kutuondolea aibu katika ujenzi wa miradi ya maji vijijini. Ombi langu kwenu sote mliopo hapa ni kuendelea kuongeza bidi, weledi na uadilifu katika kusimamia miradi ya maji nchini na katika kutekeleza majukumu yetu kwa ujumla ili tuweze kuyafikia malengo ya kitaifa katika katika sekta yetu ya maji.

**Ndugu washiriki,**

Ninatambua pia mkutano huu wa leo unahudhuriwa na Maafisa Maji wa Bodi za Mabonde yetu tisa ya maji hapa nchini. Niwashukuru waandaji kwa uamuzi wa mzuri wa kuwakutanisha hapa leo wadau wote muhimu wa sekta ya maji, wakiwemo maafisa wa bodi za maji, ambao ndio waliokabidhiwa jukumu la kulinda na kuendeleza raslimali za maji nchini.

**Ndugu Washiriki,**

Kama mnavyofahamu, **Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015-2020** inatuagiza tuhakikishe kuwa ifikapo **mwaka 2020** upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi

unafikia **asilimia 95** kwa Miji Mikuu ya Mikoa, **asilimia 90** kwa Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Maeneo yanayohudumiwa na Miradi ya Maji ya Kitaifa na **asilimia 85** maeneo ya vijijini.

Kama taarifa ya Katibu Mkuu ilivyoeleza, hatua kubwa imeshapigwa katika kufikia malengo haya, lakini pia safari bado ndefu tuendako. Sisi viongozi wenu tunaamini kabisa kuwa kwa idadi ya miradi ya maji inayoendelea mijini na vijijini, na kama tukiendelea kulinda na kuendeleza vyanzo vyetu vya maji vizuri, malengo haya yanafikika kabisa katika muda uliobaki.

**Ndugu Washiriki,**

Katika ziara zetu tumekutana na changamoto nyingi katika utekelezaji wa miradi wa miradi ya maji. Ipo miradi iliyosanifiwa na kuanza kutekelezwa siku nyingi, hasa katika maeneo ya vijijini. Ipo pia miradi ambayo imetekelezwa na kudaiwa kukamilika lakini maji hayatoki au haina uendelevu uliotarajiwa. Miradi hii imekuwa ikisababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na hata Viongozi wa juu wa Serikali. Miradi hii haipo mingi. Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu, ipo miradi 153 kwa upande wa vijijini na miradi sita (6) kwa upande wa maji mijini. Ni miradi michache lakini ndiyo inayoichafua sekta nzima ya maji.

Nitumie nafasi hii kuwaelekeza watendaji wote wanaohusika na miradi hii kuhakikisha kuwa changamoto zilizopo zinatatuliwa na miradi hii inakamilika kabla ya bajeti yetu ijayo kusomwa bungeni. Hatutaacha kuchukua hatua kali sana kwa yeyote ambaye atakwamisha juhudi zetu za kuhakikisha miradi hiyo inakamilika na kuleta tija kwa wananchi.

**Ndugu Washiriki,**

Kuna suala pia la upotevu wa maji. Taarifa ya mwezi wa Septemba 2019 inaonesha kuwa zaidi ya wastani wa **asilimia 30** ya maji yanayozalishwa yanapotea njiani kabla ya kuwafikia wananchi. Kiwango cha upotevu wa maji ni kikubwa zaidi kwa baadhi ya mamlaka nchini. Tena kwa baadhi ya miji hapa nchini wananchi wamekuwa wakilalamikia kuona maji yanamwagika barabarani kwa muda mrefu bila hatua stahiki. Kwa baadhi ya wananchi wengi wanalalamika kuwa wamekuwa wakitoa taarifa za uvujaji wa maji kwa Mamlaka zenu lakini hakuna hatua za haraka zinazochukuliwa na hatua huchukuliwa tu pale ambapo viongozi wa juu wa kitaifa au katika ngazi za mikoa wakitoa taarifa. Jambo hili halikubaliki na ni muhimu likome. Katika ulimwengu wa leo wa teknolojia hatutarajii uvujaji wa maji uendelee kwa muda mrefu bila kujulikana na hatua stahiki kuchuliwa.

Ikumbukwe kuwa upotevu wa maji ni mojawapo ya sababu za makusanyo hafifu ya maduhuli katika Mamlaka zenu. Kutokana na hali hiyo, Mamlaka nyingi zimeshindwa kulipia gharama za uendeshaji, ikiwa ni pamoja na ulipaji wa ankara za umeme kwa TANESCO. Hivyo, ninawaagiza Watendaji Wakuu wote wa Mamlaka za Maji nchini kuhakikisha kuwa mnaandaa na kutekeleza Mikakati ya Kupunguza Upotevu wa Maji katika maeneo yenu ili kufikia viwango vilivyoainishwa kwenye Mkataba wa Makubaliano ambao tumesaini kati ya Wizara na Mamlaka zenu.

**Ndugu Washiriki,**

Kama mnavyofahamu, hivi karibuni tumefanya mabadiliko makubwa katika watendaji wa baadhi ya mamlaka. Ninapenda mjue kuwa tutaendelea kufanya mabadiliko kila inapobidi. Kigezo changu kikubwa kabisa ni kiwango cha makusanyo. Ninapenda kabisa jambo hili lieleweke kwa wakurugenzi wote wa mamlaka kwamba ukiyumba katika jambo hili la makusanyo hatutaelewana. Ninasisitiza jambo hili kwa kuwa ninatambua kabisa kuwa mamlaka zetu za maji zina uwezo mkubwa wa kukusanya mapato. Muhimu ni usimamizi mzuri na kuendelea kuimarisha weledi na uaminifu.

Hata hivyo ninawapongeza wakurugenzi watendaji. Wengi mnafanya kazi vizuri na mnaanza kuelewa wizara inataka nini. Makusanyo yameanza kupanda kwa mamlaka nyingi. Ninatambua katika kipindi hiki cha mvua makusanyo yanaweza kuyumba kidogo kutokana na kupungua kwa matumizi ya maji. Lakini hiki kisiwe kisingizio cha kurudi nyuma.

Niwakumbushe pia kila Mamlaka ihakikishe kuwa inajipanga vizuri kukidhi mahitaji ya maji kwa viwanda vilivyopo na vitakavyojengwa katika kuendana na azima ya serikali ya awamu ya tano ya kuendeleza uchumi wa viwanda. Kwa hivyo, mamlaka lazima zihakikishe kuwa zinaweka mipango maalum ya kuhakikisha kuwa viwanda vyetu vinapata maji ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji.

**Ndugu Washiriki,**

Katika maeneo mengi nchini kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi na kwa Waheshimiwa Wabunge juu ya uhalali wa ankara za maji zinazoandaliwa na Mamlaka zenu. Baadhi ya wateja wamekuwa wakilalamika kuandikiwa kiasi kikubwa cha fedha kwenye ankara ambacho kwa namna yoyote ile hakilingani na matumizi halisi ya maji. Wakati mwingine ankara za maji zimekuwa zikitolewa hata nyakati ambazo huduma ya maji

haikutolewa. Sasa msitumie mwanya wa maelekezo ya wizara ya kuongeza mapato kuanza kuwabambikizia wananchi Ankara za maji. Kuwapa wateja ankara zisizostahiki ni dhambi na tutaoa adhabu kali sana kwa mamlaka yeyote itakayothibitika kubambikizia wananchi ankara za maji.

Aidha, nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wanaopata huduma ya maji kutoka kwa mamlaka zetu kuendelea kutoa ushirikiano katika kulipa ankara za maji. Ni vizuri wananchi watambue kuwa mamlaka zetu zinaendeshwa kwa Ankara wanazolipa. Pia mamlaka zinatumia makusanyo wanayopata katika kupanua mtandao wa huduma wa maji ili wananchi wengi zaidi waunganishwe na kupata huduma. Sasa tusiwe wachoyo tukishapata maji na kuanza kuwa wabishi wa kulipa maji. Wananchi wengi sana hutumia pesa nyingi kutafuta maji kabla hawajaanza kupata maji kutoka kwa mamlaka zetu. Lakini wakishaunganishwa hujisahau.

**Ndugu Washiriki,**

Ningependa nimalizie hotuba yangu kwa kusisitiza sana umuhimu wa kulinda vyanzo vya maji. Uhai wa taifa letu kwa miaka mingi ijayo utategemea sana utayari wetu leo wa kulinda vyanzo vya maji. Bahati mbaya sana vyanzo vingi vimevamiwa na

wananchi ama kwa kilimo au makazi. Jambo hili halikubaliki na tunaendelea kuwasisitiza wananchi kuacha mara moja kulima au kujenga katika vyanzo vya maji.

Bodi za Mabonde ya Maji ndizo zilizokabidhiwa jukumu la kutekeleza sheria ya usimamizi wa raslimali za maji. Hata hivyo, usimamizi wa jukumu hili umekuwa hauridhishi pengine kw sababu tumekuwa tukiweka mkazo mkubwa katika eneo la usambazaji wa maji, ambapo ndipo macho ya wanasiasa wengi yalipo. Kuanza sasa tutakuwa tunachukua hatua kali sana kwa Bodi zote za mabonde pale ambapo tutakuta wananchi wamevamia vyanzo vya maji kwa kulima au kujenga bila hatua stahiki kuchukuliwa.

**Ndugu washiriki,**

Ninapenda tena kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuruni tena kwa kazi kubwa mnayoifanya katika kuendeleza sekta ya maji. Tuendelee kushirikiana na kupendana na kudumisha bidii, weledi na uadilifu. Tuna jukumu kubwa katika kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na maji na maji haya yanasambazwa kwa wananchi kwa matumizi mbalimbali. Tunaweza. Maji Bombani lazima yafike!

Sasa ninayo furaha kutamka kuwa mkutano huu wa watendaji wakuu wa Wizara ya Maji na taasisi zake umefunguliwa rasmi.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**